JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 444

# UDPS/Sud-Kivu yaleta uwasiwasi

Tangu hapo bwana Faustin Birindwa ateuliwa kunako "conclave" ya Kinshasa kuwa waziri mkuu, mambo hayaendeki barabara kunako UDPS/Sud-Kivu. Wengi wahakikisha kuwa kuna mchafuko mkubwa kunako UDPS, baazi ya viongozi wake jimboni huwa na hali ya kibaridi na ya ukimya.

Na hali hiyo yaleta uwasiwasi kwa wapendelevu wa chama hicho. Ili kuwaeleza zaidi wasomaji wake, gazeti JUA kapendelea kusikia maoni ya vijana wa BBC/Carrefour ambao waonekana kuwa kiini (noyau) mtaani Kadutu wa wakaaji kuhusu mambo ya siasa. Na ambao wengi kati yao ni wanamemba wa UDPS.

Maoni ya vijana hao katolewa na bwana Kakusu Jean D'arc aliye katibu ahusikaye na mipango pia usalama kunako "BBC"(hiyo ya Carrefour).Kwa jina la kundi hilo, bwana Kakusu kanena ya kuwa UDPS ni chama cha mabishano makubwa sasa. Tangu hapo Birindwa alipochaguliwa na kuwabeba mashabiki (fanatiques) wake kama vile Biringanine na Guhanika ambao waliotuuzi kila mara kwenye redio ya kama watu wasiunge mkono serkali isiyokubaliwa na HCR.

Hata hivyo, mabwana hao hawakusema lolote juu ya Bwana Birindwa kukubali kuunda serkali mpya ingawa umma halikuwa hakika na jambo lile. Ni wakati tu hawakuweza kupata nafasi katika Baraza la mawaziri ndio wakaanza kutoa maoni yao. Aibu sana ! Kwa mshangao mkuu wakaaji kasikia kama bwana Magabe na Biringanine kajielekeza mjini Kinshasa kukutana na yule ambaye Jimbo la Kivu ya Kusini yaita " Yuda Iskarioti". Zaidi ya yote, waliporejea mjini Bukavu maneno yao yakaonekana ya unafiki. "Tuunge mkono serkali inayohusika na maisha ya raia", wakisahau kama Nguz na Mungul Diaka walijiruhusu pia kutamka maneno yale. Kwanza, walipotoka mjini Kinshasa, mkusanyo wao na wanamemba wa chama haukufaulu, watu kagawanyika. Pili, ujumbe wa Magabe na Biringanine kakataliwa na wanamemba wa UDPS. Tatu, kiongozi wa chumba cha waziri mkuu Tshisekedi kanena kuwa hakuweza kuwafuata kwenye redio na televisheni. Na ndipo twasema kama wamekwisha kuwa watu wauongo kama wategemea siasa " ya mouvance présidentielle". Ine, ndugu hao wakataa kuitisha mkutano wa wanamemba kwa sababu vijana na wazee wa UDPS wapendao mabadiliko wapendekeza kama warushwe madarakani.

Tano, hawachukue hatua yoyote ili kumuondoa Guhanika katika UDPS. Kwa nini ndugu hao hawakusema lolote kama wenzio Chimanuka na Pierre Lumbi ? Ni kweli kama kakosea na hawana tena pongezi la "BBC". Na wangejua tangu leo eti UJDR (union des jeunes démocrates pour la reconstruction) yaunga mkono mwanasiasa yeyote ule aliye upande wa mabadiliko na asiyenaswa mtegoni na azibitishe yale kwa matendo yake.

Kwa vile Lukama, Kasele, Anzuluni, Ramazani, Kyembwa, Birindwa, Guhanika, Magabe, Biringanine kakosea umma la Sud-Kivu, watu wamekuwa wakengeufu (détournés). Pamoja na hayo, twawatia moyo wanamemba wa UDPS kuchukua hatua zao zote ili kuzibiti hali ya chama kwa sasa.

**Mutungwa Abandelwa Phély**

## UHARIRI

# Vyama na demokrasia

Iliruhusiwa kusimikwa nchini Zaïre siasa ya vyama vingi. Na kwa kweli kukaundwa vyama vya kisiasa mamia na mamia. Kitendo hicho kikategemea zaidi ukabila, majimbo na vita mambo ambayo yawachonganisha raïa na kutia vilio katika jamaa, makao, mashamba, duka na viwanda kuharibishwa ao kuchomwa. Na toka vitendo hivyo haramu, ndugu wengi hutezamiwa kama vile wakimbizi wa siasa mahali mengi nchini mwao wasijue la kufanya. Na ni hapo watu wengi nchini mwao wasijue la kufanya.

Na ni hapo watu wengi hawaaminie tena siasa hiyo na mabingwa wake kama vile walikuwa wakitumainia mambo yaendeshwe. Kweli mwangaza wa demokrasia upo mbali kwa kuwaangazia

Wana-zaïre wote. Mwangaza uliohitajika kweli umepambana na kuzibwa na magumu mengi. Na raïa, baada ya kujigawa, wahuzuria vurugo lilioko, uharibifu wa mambo, kuzorota kwa hali ya ujamii na ya uchumi. Demokrasia, dawa ya kuleta nguvu na kusisimua, ambayo yaletwa na siasa ya vyama vingi mahali mengine, yageuka siku kwa siku msinji wa utokubali na uwasiwasi.

Kwa kweli, kutokana na hali ya kisiasa iliyoko nchini kwa sasa, siasa ya vyama vingi imesimikwa kweli, lakini Wana-Zaïre wangojea mradi wa umma ulio wa kweli na wa kudumu. Ule ambao utaweza kuinua hali ya kijamii na ya kiuchumi. Isiwe tu ahadi za mabadiliko ambazo hazitatimizwa baadae. Kwa hayo wasema na majawabu kwa matatizo yaliyoko ummani kwa sasa. Yabaki na Wanasiasa hawasikii hayo ingawa ndio wanao uwezo juu ya raia na wajifurahisha kupiga kauli na kelele, kuwahotubia watu maneno ya sukari ijapokuwa walinda na wakinga faida zao pekee.

Oni hilo laelekea sio tu mabingwa na wengineo wana siasa bali pia raïa wote Wana-Zaïre ambao ubora na urahisi wa hali yao ya kijamii na ya kisiasa nchini yawaelekea kabisa.

Mambo ni muhimu na makubwa. Kumbe yafaa raïa wote wahusike kweli wenyewe na hali yao. Na wakubali kutimiza mambo yanayowaelekea kwa kufikilia hali bora ya maisha inayohitajika. Yawezekana kweli kuundwe vyama vingi na siasa ya demokrasia isisimikwe kama ifaavyo nchini kama mwananchi hana uhuru, haki na uwezo wa kufuata na kuunga mkono siasa hiyo, kama sheria haipo bora na huru, kama mapendo kwa nchi na raïa haitiwe juu ya faida ya hayo twashiriki.

**André Bisimwa L-B. Tserou**

# Wakaaji wapenzi wa zone ya Masisi, Walikale, Rutshuru, Nyiragongo na Goma

Wakubwa wa jimbo la Kivu ya Kaskazini (Nord-Kivu) wakishirikiana na wale wa kabila zenyi kuishi katika jimbo hilo, wanawaomba nyinyi wote kuacha vita na uchokozi wowote sawa vile ilivyoamriwa na vice-premier ministre et ministre de l'intérieur wakati alipita hapa Goma tarehe 14 mai 1993. Tangu leo, atakayechokoza mwenzake ataazibiwa vikali sana.

Amani, mapendo na masikilizano kati ya makabila zote jimboni ni vya lazima kwa maisha na maendeleo ya jimbo letu la Nord-Kivu.

Mutembo, Muhunde, Munyanga, Muhutu, Mukumu, Mututsi, Munande na wengine wote tupo wandugu ! Tuache vita, kuuana na kuchomeana nyumba na kuharibishiana mali zetu.

Tunawajulisha kama wowote ataleta tena fujo juu ya kabila na kufukuza mwengine wala kumushambulia ao kunyanganya mali ya wengine atahukumiwa vikali sana kufuatana na sheria. Mwenyezi Mungu atulinde. Imefanyika pa Goma, tarehe 24 mai 1993Pour la région du Nord-Kivu

**Le gouverneur de région**
Jean-Pierre Kalumbo Mbogho

**Pour les communautés ::**
- Hunde : 1. Ndyanabo Buunda; 2. Hangi Kuba
- Nande : 1.Kambale Ndeti Kagephar; 2. Kahindo Tey Tey
- Nyanga : 1. Baruku Matekere; 2. Miroza Muriki
- Tembo : 1. Shomwa Mongera; 2. Ngulu Wete
- Hutu : 1. Nzabara; 2. Gatambi
- Tutsi : 1. Gasana; 2. Habarugira H.
- Kumu :1. Ntibiramera R.

**- Magrivi**
1. Mashagiro
2. Rumashana